
# Pambazuko

Toleo Namba 025 Jumatatu Januari 2-7, 2023




## ●Tanzania itakuwa imesimama wapi?
## ●Rushwa, wizi vikiendelea 'twafa'

Na Simon Martha MKINA

MIAKA 10 ijayo – hadi kufikia mwaka 2033, Tanzania itakuwepo. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan hatakuwa madarakani, huku idadi ya watu ikikadiriwa kuwa zaidi ya milioni 75. Je, uchumi wake utaimarika na maisha ya watu kuwa bora zaidi?

Habari Zaidi Uk. 10

# Bakhresa, Mo Dewji, Rostam Aziz watajwa

Uk. 7

JISAJILI HAPA: Andika neno HABARI na tuma kwenye namba hii ya WhatsApp - 0744 768263 kupata gazeti bure

# Tuko 284,427. Aksanteni

AWALI ya yote tunapenda kuwatakia wasomaji wetu heri ya mwaka mpya wa 2023. Tunaamini utakuwa mwaka wenye neema na baraka tele kuliko ilivyokuwa mwaka ambao uliishia juzi – Jumamosi Desemba 31, 2022.

Tunaamini kwamba mazonge na madhila yaliyoikumba nchi na kusababisha madhara makubwa, hayatatokea tena – labda yale yaliyo juu ya uwezo wa binadamu kuyakabili.

Hata hivyo, bila kujali yepi yamo ndani ya uwezo wa binaamu au la, basi kila mabaya yaliyotokea mwaka jana yawe funzo kubwa kukabili na kuepusha hasara ya mali na nguvu kazi kwa mwaka huu.

Wakati toleo hili ndiyo la kwanza kwa mwaka huu – baada ya kuendelea kuufikia umma kwa miezi sita bila kukwama, tunapenda kuchukua fursa hii kuwapongeza sana wasomaji wetu, wachangiaji wa makala, safu na vibonzo, waliotupa ushauri na wapenzi wote wa Pambazuko kwa ujumla wake.

Miezi sita iliyopita wakati tukianza gazeti hili linalotolewa bila malipo kila wiki, wengi walidhani ni ndoto, maswali yakawa mengi; mengine ya kukatisha tamaa, lakini kwa kuwa tulikuwa na nia, lengo limetimia na tunaendelea kuimarika na kusonga.

Katika kipindi hiki cha miezi sita, habari nyingi zimeandikwa kwa weledi mkubwa, picha nyingi zimetumika, katuni na vibonzo vimesheheni, makala zenye kuelimisha na kukanya yameandikwa na zaidi sana safu zetu zimeendelea kuwa bora zaidi.

Tunawashukuru sana watu wote wanaoendelea kututia moyo kwamba, pamoja na kusambaza gazeti bure, ubora wa yale yanayochapwa na Pambazuko hauna shaka hata kidogo, ndiyo maana gazeti linaendelea kupendwa na kusambazwa zaidi na zaidi.

Katika kipindi hicho chote, zaidi ya habari na makala 600 yamechapwa na Pambazuko na matokeo ya habari hizo yanaweza kupimika – kwa maana ya kusukuma hatua kuchukuliwa.

Moja ya habari kubwa ambayo matokeo yake yamepatikana haraka na yanapimika ni habari kubwa iliyoandikwa Desemba, 2022 iliyokuwa ikielezea namna Wizara ya Afya inavyokwamisha ustawi wa afya kwa Watanzania kwa kushindwa kutoa leseni kwa hospitali binafsi, licha ya kukamilisha taratibu zote na baada ya kukaguliwa na wizara hiyohiyo.

Baada ya habari ile wiki iliyofuata, wizara ilianza kutoa leseni na bado inaendelea kutoa kwa hospitali binafsi zilizokidhi viwango.

Pamoja na matokeo hayo, na wakati tukianza mwaka mpya wa 2023, tunahimiza serikali, taasisi, jumuia, ofisi zote na zile za binafsi kufanya kazi kwa bidii kwa kuwatumikia vyema Watanzania ili kuwa chachu ya kukuza uchumi wa familia na taifa.

Pambazuko tunasema tena, aksanteni sana kwa kuwa pamoja nasi kwa miezi sita hata kutufanya kuwa chombo kinachosambazwa na kusomwa zaidi Tanzania.

Sasa familia ya Pambazuko inawafikia watu 284,427 kila wiki bila kukosa.

Endeleeni kutuunga mkono ili tuboreshe zaidi kazi zetu.




## Jisajili kupata Pambazuko bure

- Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa namba hii ya simu ya **WhatsApp: +255 744 768263** kwa kutuma neno **"HABARI"** kwa namba yako ya WhatsApp ili kupata Pambazuko kwenye WhatsApp yako.
- Pia unaweza kujisajili kwa kutumia **Email hii: pambazuko1@protonmail.com** ili gazeti la Pambazuko likufikie kupitia email yako, andika neno **"HABARI"** na kutuma kwetu nawe utakuwa umejisajili.

## *NUKUU*



***Napenda kuwakumbusha viongozi wenzangu, tuliobeba jukumu zito la kuhudumia taifa hili, kwamba Watanzania wana matumaini makubwa kwetu na kwamba tunatarajiwa kuendelea kuliongoza taifa hili kwa juhudi, uadilifu na kwa misingi ya haki na sheria – Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan - Desemba 31, 2022, wakati akituma salamu za mwaka mpya 2023.***

# Lala salama Papa Benedict




**Na Mwandishi WETU**

PUMZI ya binadamu anayesifika kuwa kiongozi msomi na mjuvi wa hali juu wa sheria, kanuni na taratibu za Kanisa Katoliki duniani, Papa Benedict imekoma.

Amefariki dunia akiwa na miaka 95, akiwa ndiye kiongozi anayetajwa kuwa na uelewa mkubwa wa historia, mienendo na misimamo ya Kanisa Katoliki.

Papa Benedict wa 16, ambaye jina lake halisi ni Joseph Aloisius Ratzinger, raia wa Ujerumani alipata shahada ya uzamivu katika theolojia na shada nyingi za udaktari wa heshima, aliaga dunia siku ya mwisho kabisa ya mwaka – Jumamosi, Desemba 31, 2022, akiwa Vatican City. Sababu za kifo chake ni uzee na kuzorota kwa afya yake.

Kabla ya kuwa kiongozi mkuu wa kanisa hilo linaloaminika kuwa na waumini na wafuasi wengi duniani, alipitia nafasi nyingi za utumishi na uchungaji, hata kukwea ngazi ya uongozi kuwa msaidizi na msiri wa Papa Yohane Paulo wa Pili, nafasi aliyoitumikia kwa umakini, weledi na staha ya hali ya juu.

Sifa za utendaji wake zilisambaa na kukomazwa kwa namna alivyohimili maisha ya Upapa ya Yohane Paulo wa Pili wakati wa madhila ya kushambuliwa na hata kuumizwa kwa risasi. Huyu ndiye alikuwa msaidizi maalum na mtu aliyebeba majukumu makubwa ya kuongoza Kanisa Katoliki wakati Papa akiwa kitandani.

Amekuwa akisifika kuwa na maono juu ya uhai wa Kanisa hilo na kwamba hakupenda sana kila mabadiliko yanayotokea yaakisi Ukatoliki.

Huyu alikuwa mwiba kwa wakosoaji wa kanisa, maana anaelezwa kuwa na utetezi wenye mashiko ambao, wakati mwingine uliwaacha "hoi" waliokuwa wakihimiza mabadiliko ya uendeshaji wa kanisa hilo na hata maisha ya Ukatoliki.

"Papa Benedict, alikuwa na hoja nzito, wengi waliokuja na mawazo ya mabadiliko, baada ya kukutana naye ama kusoma waraka wake, waliishia kukubali," inasomeka moja ya maoni waombolezaji wa kifo chake kupitia Twitter.

Papa Benedict hadi kifo chake amekuwa mtetezi mkuu na mlezi wa mtazamo wa imani wa Kanisa Katoliki kuhusu masuala ya kutoa mimba na uzazi wa mpango.

Joseph Aloysius Ratzinger alizaliwa katika familia ya kikatoliki Aprili 16, 1927, katika Jimbo la Bavaria, Ujerumani.

Alichaguliwa kuwa kiongozi mkuu wa kanisa hilo Aprili 19, 2005 na kutawazwa kuwa Papa akichukua jina la Papa Benedict wa 16.

Upapa wake ulidumu miaka nane tu kwani Februari 28, 2013, aliamua kuachia ngazi kwa hiari yake akieleza anafanya hivyo kutokana na "kuishiwa nguvu kwa uzee na kunyemelewa na magonjwa."

**Alale salama Papa Benedict wa 16.**

# Gazeti lafanikisha leseni 63

Na Mwandishi WETU

HATIMAYE Wizara ya Afya imeanza kutoa leseni 63 za kuanzisha hospitali binafsi zilizokwama mezani kwa waziri wake, Ummy Mwalimu.

Leseni hizo – nyingi zikiwa zimekaa miezi hadi tisa, zilikwamisha kuanza ama kuendelea kwa huduma za afya maeneo jirani zaidi na wananchi.

Mmoja wa wamiliki wa hospitali binafsi ameliambia Pambazuko jana kuwa "tunashukuru sana waandishi wa Pambazuko kwa kupigania haki, na sasa ninavyozungumza nimepatiwa control namba (namna ya kulipa malipo ya serikali) ili nilipe nipewe leseni yangu."

Pambazuko limeona karatasi inayomtaka kulipa kiasi cha Sh. 1,700,000 anachotakiwa kulipa mwekezaji huyo ili apate leseni.

Ameonyesha kufurahishwa kwake na namna Pambazuko lilivyoandika na kufuatilia kadhia hiyo na hatimaye wizara imetenda haki.

Gazeti hili, Pambazuko katika toleo lake la Desemba 12-18, 2022 liliandika habari kubwa ukurasa wa kwanza ambayo ilikuwa ikieleza namna huduma za afya zinavyokwamishwa na wizara husika.

Katika habari hiyo ya uchunguzi, Pambazuko lilibaini kuwa mezani kwa waziri, leseni hizo hazikufanyiwa kazi, kiasi cha kuendelea "kuumiza" watoa huduma – wawekezaji, huku wagonjwa wakikosa haki yao ya kupata matibabu jirani zaidi na makazi yao.

Mbali na kukwamisha, wizara hiyo ilikuwa inaikosesha serikali mapato amayo kutokana na eseni tu, ilikuwa inapata kiasi kinachofikia Sh. milioni 107, 100,000 kutokana na gharama za kupata leseni mpya kuendesha hospitali binafsi.

Gazeti la Pambazuko katika habari ile, lilieleza kwamba wizara hiyo ilijiingiza katika kashfa ya kukwamisha ustawi wa huduma za ushauri na uchunguzi wa afya na matibabu.



*Ummy Mwalimu, Waziri wa Afya*

Kashfa hiyo inatokana na wizari hiyo kuchukua zaidi ya miezi tisa kutoa leseni za kuanzisha hospitali binafsi, licha ya kupitishwa na ofisi na bodi ya udhibiti.

Kufuatia ucheleweshaji huo, huduma za afya nafuu na jirani na wananchi zinakosekana na kuwa chanzo cha madhila makubwa kwa wananchi wanaokabiliwa na magonjwa, ikiwamo vifo.

Pambazuko lilipata taarifa kwamba ndani ya makao ya wizara hiyo, jijini Dodoma kuna leseni 63 ambazo zimekwama, licha ya kutakiwa kusainiwa na kukabidhiwa kwa wahusika ili kuendelea na kutoa huduma za afya.

Inadaiwa kuwa idadi hiyo ya leseni "zilizokaliwa" wizarani hapo zinatoka mikoa tisa.

Uchunguzi uliofanywa na Pambazuko ulibaini kuwa hospitali hizo mpya zimekamilisha taratibu zote za kupewa leseni hizo kwa muda mrefu, lakini hadi wakati huo hakuna aliyepewa.

Sheria ya Hospitali Binafsi iliyosainiwa na Rais wa Kwanza wa Tanzania, Julius Nyerere na kuanza kutumika Juni 22, 1977, inaeleza kuwepo kwa hospitali hizo na umuhimu wake umekuwa ukionekana kwa kuwa msaada mkubwa wa kuokoa maisha ya watu.

# DC mbabe kufidia milioni 80/-

**Na Mwandishi WETU**

UONEVU na matumizi mabaya ya madaraka yamekemewa vikali na mahakama na kutoa mfano kwa kuamuru mkuu wa wilaya kulipa fidia ya Sh. milioni 80 kwa kudhalilisha mwananchi.

Hakimu Mkazi Mkoa wa Tabora, Jovith Kato imetoa hukumu kwa aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Tabora Mjini, Komanya Kitwala kumlipa fidia ya kiasi hicho cha fedha milioni 80, Alexander Ntonge mkazi wa Kata ya Ipuli, Tabora Mjini.

Sababu ya hukumu hiyo ni baada Kitwala kupatikana na hatia katika mashitaka aliyofunguliwa ya kuwaamuru polisi kumkamata Ntonge na kumdhalilisha mbele ya familia na majirani.

Akisoma hukumu hiyo katika shauri la madai namba 4 la mwaka 2021, Hakimu Mkazi, Jovith Kato alisema mahakama imepitia ushahidi wa pande zote mbili na kujiridhisha kwamba Komanya Kitwala alitenda kosa hilo Januari 5 mwaka 2020, na hivyo mahakama imemuhukumu kulipa shilingi milioni 80 badala ya shilingi milion 140 ambazo mlalamikaji alidai kulipwa kutokana na makosa ya udhalilishaji.

Awali, wakili wa mlalamikaji, Kelvin Kayaga aliiambia mahakama kuwa Komanya Kitwala alikwenda nyumbani kwa mlalamikaji akiwa na polisi ambao aliwaamuru kumkamata na kumtesa, kisha kumuweka ndani katika Kituo Kikuu cha Polisi Tabora Mjini bila kuwa na kosa lolote.

Akiwa amekaa kwa muda katika kituo hicho, baadaye aliyekuwa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tabora kwa wakati huo, ACP Safia Jongo aliagiza mlalamikaji Alexander Ntonge kuachiliwa huru kwa madai hakuwa na kosa lolote alilofanya.

Katika mlolongo wa kesi hiyo iliyokuwa ikivuta hisia za wananchi wengi, mapingamizi mengi ya Kitwala yalikuwa yakitupiliwa mbali baada ya kushindwa kuishawishi mahakama kwamba hakuwahi kumdhalilisha mlalamikaji.



*Komanya Kitwala*

Mahakama hiyo ilielezwa kwamba kwamba mdaiwa alimdhalilisha mteja wake Alex Ntonge Januari 05/2021.

Kwamba siku hiyo mdaiwa Kitwala Komanya akiwa Mkuu wa Wilaya ya Tabora akiwa ameambatana na polisi walifika nyumbani kwake na kumdhalilisha mlalamikaji.

Kwamba mdaiwa akiwa na askari hao wenye silaha baada ya kufika nyumbani hapo walimkamata mdai Alex Ntonge na kisha walimfanyia vitendo vinavyodhalilisha utu wake mbele ya familia na majirani.

Kitwala ambaye analazimika kulipa fidia hiyo binafsi, aliengulіwa nafasi ya mkuu wa wilaya na Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan Juni 19, 2021.

Mkuu huyo wa wilaya aliwahi kushutumiwa na chama chake, Chama Cha Mapinduzi (CCM) kwamba anatishia uhai wake chama hicho Tabora kwa kuendekeza kile kilichoita "ubabe."

Juni, 2020 chama hicho kilipiga kelele kumkemea mkuu huyo wa wilaya kwa kutumia nguvu isiyohitajika kuwalazimisha wafanyabiashara wadogo kulipia vitambulisho vya mjasiriamali.

CCM ilidai kuwa mkuu huyo wa wilaya alikuwa akitumia Polisi wenye silaha katika shughuli zake nyingi, hivyo kuhatarisha ushindi wa chama hicho katika uchaguzi mkuu uliokuwa ukifanyika mwaka huo.

# Bakhresa, Mo, Rostam watajwa

**Na Scovya MANASE**

WAFANYABIASHARA wakubwa watatu wa Tanzania, ni miongoni mwa matajiri wenye viwanda vingi Afrika.

Mbali ya kumiliki viwanda, wanatajwa pia kuwa miongoni mwa watu wenye ukwasi mkubwa na kwamba wanaongoza kwa kuajiri idadi kubwa ya watu.

Wanaotajwa na jarida jipya la Marekani, The Loaded - toleo la Afrika, linalotarajiwa kuchapishwa baadaye mwezi huu, ni pamoja na Salim Bakhresa, Mohammed Dewji na Rostam Aziz.

Majina haya ya matajiri zaidi wa Tanzania, ndiyo yamekuwa yakitajwa mara kwa mara na vyombo kadhaa vya habari duniani vinavyofuatilia taarifa za ukwasi wa watu maeneo mengi duniani.

Jarida la The Loaded, lenye mwelekeo wa habari zake kama ilivyo Forbes, litaanza kutoka mapema mwaka huu na linasimamiwa na waandishi kadhaa kutoka Marekani, baadhi ya nchi za Afrika, Uingereza, Canada, na India.

Katika Tanzania, gazeti hilo linashirikiana kikazi na gazeti la Pambazuko na limekuwa mwakilishi kwake katika nchi za Kenya, Uganda, Rwanda, Malawi na Burundi.

Matajiri hao wa Tanzania, pamoja na kwamba The Loaded litataja utajiri wao, lakini Pambazuko linaweza kueleza kwamba wote hao ukwasi wao unatokana na kumiliki viwanda vya kuzalisha vyakula, sukari, bidhaa za karatasi, vinywaji, kufungasha gesi ya majumbani, bidhaa za ngozi, nguo na vinginevyo.

Bakhresa, kama ilivyo kwa Dewji, ana miliki viwanda nje ya Tanzania, hasa katika nchini za Malawi, Afrika Kusini na kuna tetesi mmoja wao atakuwa na kiwanda cha kuzalisha vyakula Rwanda.

Jarida la Forbes katika toleo lake moja la 2015, liliwahi kuandika kwamba Dewji, ndiye alikuwa tajiri zaidi kijana katika ukanda wa Afrika.

Anayetajwa hadi leo kuwa ni nambari wahedi katika utajiri Afrika ni Aliko Dangote, kutoka Nigeria ambaye anamiliki viwanda vya kusindika vyakula, saruji, uzalishaji wa sukari na bidhaa nyingine nyingi. Anaelezwa kuwa na viwanda katika nchi 20 za Afrika. Bara la Afrika lina nchi 54, likiwa na idadi ya watu wanaokaribia bilioni 2. Dunia ina watu takribani bilioni 8.


*Rostam Aziz*

Takwimu za wenye ukwasi mkubwa duniani, Dangote anatajwa kuwa na zaidi ya dola za Marekani bilioni 12 na kuongoza Afrika kwa utajiri, huku akishika nafasi ya 144 duniani kwa kumiliki kiasi kikubwa cha fedha na mali.

Anayetajwa kuwa tajiri zaidi duniani ni Mfaransa Bernard Arnault ambaye ni mmiliki wa kampuni zinazojihusisha na kutengeneza mavazi yenye gharama kubwa na vinywaji aghali zaidi duniani. Kampuni yake inaitwa LVMH (Moët Hennessy Louis Vuitton). Anaelezwa kuwa na utajiri unaofikia dola za Marekani bilioni 180.8.

# Misingi ya haki za kijamii

**Na Askofu Dkt. Stephen MUNGA**

BAADA ya kuandika makala mfululizo juu ya demokrasia na nguzo zake ni vyema sasa kuangalia eneo lingine ambalo linatunza hazina kubwa ya fikra za kimabadiliko na kimatengenezo.

Hili ni eneo la haki za kijamii. Eneo hili limekamata usikivu wa wanaharakati na wanazuoni wa haki za binadamu kwa nyakati zetu.

Harakati za kutetea haki za kijamii zimekuwa chimbuko la ukombozi kisiasa, kiuchumi na kijamii kwa jumla. Lakini, pia zimekuwa chimbuko la kutungwa kwa sheria na maazimio mbalimbali ya kulinda haki za watu katika jamii.

Historia ya dhana ya haki ya jamii inaanza na Mjesuti wa Kiitaliano, Luigi Tapparelli d'Azeglio. Yeye alianzisha neno hili kama dhana ya kiuchumi akionyesha ukosefu wa usawa na dhiki ya kiuchumi iliyosababishwa na mfumo wa tabaka za kijamii huko Ulaya.

Alitumia wazo la mwanafalsafa wa Italia, Thomas Aquinas katika kujenga dhana hii; mkazo mkubwa hapa ni kuwa pamoja na kufanya jambo sahihi, tunapaswa kujitahidi kufanya kile kinachohitajika kwa uboreshaji wa wengine.

Leo, dhana ya haki za kijamii mara nyingi zinarejea haki za binadamu zinazojikita katika kuboresha maisha ya makundi yaliyotengwa kihistoria kwa misingi ya rangi, kabila, utaifa, jinsia, mwelekeo wa kijinsia, umri, dini na ulemavu.

Katika makala yafuatayo tutaangalia malengo na vikwazo vilivyomo katika kutafuta haki za kijamii kupitia kanuni tano zinaonekana kuwa za msingi.

Kwa upande mmoja, dhana hii imekuwa msingi wa kujenga na kuibua hoja zilizoleta manufaa ya ukombozi kwa makundi tofauti ya watu.

Nadharia na juhudi nyingi za ukombozi, ikiwemo theologia ya




*Katiba*

ukombozi, zina mizizi katika dhana hii ya haki za kijamii. Tunaweza kudai kwamba mapambano makubwa kama vile juu ya kukomesha utumwa na ukoloni vina sura ya kubebwa na dhana hii.

Haki za kijamii ndio chimbuko la sauti zote zinazokemea ukandamizaji wa aina zote. Kwa hiyo, ni dhana inayolinda makundi yote ya watu yaliyopo na yatakayoibuka.

Kwa hiyo hii ni dhana ya matumaini kwa wote wanaoonewa na kukandamizwa kwa namna tofauti. Katika maisha ya hapa duniani hii ni dhana iliyoasilisha utunzi wa sheria mbalimbali za kimataifa na kitaifa juu ya haki za watu.

Sifa hiyo ya dhana hii kuwa msingi wa utetezi wa makundi mbalimbali yanayokandamizwa imeifanya kuwa chimbuko la misuguano katika nyakati zetu.

Kwa hiyo mijadala ya nyakati hizi juu ya haki ya kijamii katika baadhi ya maeneo yamegonga kuta za mapokeo ya kitamaduni na kidini katika jamii mbalimbali.

Hata hivyo, bila shaka tunakubaliana kuwa pamoja na changamoto mbalimbali katika ufafanuzi na matumizi ya dhana hii, bado inabaki kuwa ya msingi katika kujenga hoja za msingi za utetezi wa haki za jamii.



**Na Evarist Chahali**
evarist@chahali.com

# Tukawe watu bora zaidi 2023

NAPENDA kuwatakia heri ya mwaka mpya wasomaji wangu na hasa wasomaji wa gazeti letu la Pambazuko.

Katika moja ya makala zangu za mwaka jana katika safu hii nilieleza kuhusu "jinsi ya kuwa mtu bora", neno nililobuni mwenyewe kama tafsiri ya neno la Kiingereza "personal development."

Hii "personal development" ni miongoni mwa mada zilizotawala sana mwaka jana, na bila shaka itaendelea kutawala mwaka huu 2023 na zaidi.

Umaarufu wake umechangiwa na changamoto mbalimbali zilizoikabili na zinazoendelea kuikabili dunia yetu.

Kwa huku nchi za Magharibi, janga la korona limeacha majeraha makubwa sana. Kwa mfano, kwa hapa Uingereza, licha ya janga hilo kusababisha vifo vya watu zaidi ya laki mbili, pia limeathiri mno uchumi wa nchi hii ambayo ni miongoni mwa nchi tajiri duniani.

Na kabla majeraha ya korona hayajapona, kukaibuka vita vya Russia dhidi ya Ukraine.

Lakini yote haya, korona na vita ya Ukraine, yalijiri wakati uchumi wa dunia ukiwa haujapona kufuatia mtikisiko mkubwa wa uchumi mwaka 2008.

Kuhusu "jinsi ya kuwa mtu bora," nilieleza katika makala husika kuwa lengo hasa ni kumjengea mtu uwezo wa kutumia nyenzo alizonazo "ndani yake" kukabili changamoto mbalimbali. Au kuwa mtu "bora zaidi".

Binafsi, mbinu mbalimbali za "jinsi ya kuwa mtu bora" zimesaidia sana kukabiliana na changamoto za mwaka 2022, na ninaamini zitanisaidia mwaka huu pia.

Kwa bahati mbaya, mwaka huu unatarajiwa kutokuwa na nafuu, hasa kwenye athari ya vita ya Ukraine kwenye uchumi wa dunia.

Athari hizo zitakuwa kali zaidi kwenye



*Mwaka*

nchi zetu masikini, ambazo licha ya kutegemea misaada, matumizi yake ni ya kifahari.

Hata hivyo, miongoni mwa vitu vinavyofundishwa kwenye "jinsi ya kuwa mtu bora" ni kuziangalia changamoto kama fursa.

Kwa mfano, ugumu wa maisha unaweza kutoa fursa ya kutafakari kuhusu njia mbadala (halali) za kuongeza kipato.

Pengine afya inayumbua, na unaambiwa shinikizo la damu lipo juu. Hii inaweza kuwa fursa muhimu ya kuanza utamaduni wa kufanya mazoezi, sambamba na kuanza kula "mlo wenye faida kwa afya yako" (kwa mfano kupunguza sukari, mafuta, nk).

Hata kwenye siasa, kiu ya katiba mpya inaweza kuwa fursa ya kuamsha tafakuri kuhusu "katiba yako mwenyewe" – mfano uadilifu binafsi.

Naamini kwamba ili kuwa na taifa bora twahitaji watu bora, kwani taifa ni mkusanyiko wa mtu mmoja mmoja – ambaye anawakilisha jamii pana ambayo inaweza kuwa na watu bora, hivyo kuwa na taifa bora zaidi.

Nimalizie kwa kuwatakia tena heri ya mwaka mpya 2023.

# Tanzania miaka 10 ijayo

**Na Simon Martha MKINA**

MIAKA 10 ijayo – hadi kufikia mwaka 2033, Tanzania itakuwepo. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan hatakuwa madarakani, huku idadi ya watu ikikadiriwa kuwa zaidi ya milioni 75. Je, uchumi wake utaimarika na maisha ya watu kuwa bora zaidi?

Swali hilo linajibiwa na Watanzania walioko ndani na nje ya nchi kwa kutoa maoni yao kupitia gazeti hili la Pambazuko.

Idadi kubwa ya Watanzania 'wamejenga' matumaini na imani kwa nchi yao kwamba katika kipindi cha miaka 10 ijayo, nchi itakuwa na maendeleo makubwa.

Maendeleo wanayoyazungumza hapa ni kuwa na uchumi imara wenye kuakisiwa kwenye miundombinu bora na ya kisasa; ikiwamo barabara, shule, hospitali zenye huduma bora za afya na mazingira mazuri ya kufanya biashara.

Hata hivyo, wapo wanaoeleza wasiwasi kuhusu maendeleo hayo huku wakieleza kwamba huenda yakatingwa na baadhi ya tabia ambazo sasa zinaonekana kukomaa na kuwa za kawaida; rushwa na ubadhirifu.

Pambazuko limefanya tathmini ya utendaji wa serikali inayoongozwa na Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan na kubaini kwamba asilimia 57 ya watu waliohojiwa wamejenga imani ya "mambo mazuri kuendelea kutokea," huku wakieleza kwamba ndani ya miaka 10, Tanzania itakuwa na ustawi wenye "heri kwa idadi kubwa ya watu wake."

Imani yao inajengwa na mtazamo wa mwenendo wa utendaji wa serikali ya sasa, huku wakieleza kwamba Rais Dkt. Samia "anakwenda vizuri."

Hata hivyo, wapo watu asilimia 43 ambao wamehojiwa, ambao wameonyesha wasiwasi wao kuhusu ujio wa maendeleo makubwa katika miaka 10 ijayo, wakieleza kwamba, "matumizi ya serikali ni makubwa kupita kiasi, hivyo kuwa tishio kwa matumaini ya maisha bora kwa watu wengi zaidi."

Tathmini ya utendaji wa serikali kwa kipindi cha mwaka mmoja na maoni yao kuhusu miaka 10 ijayo, ilifanywa kwa kuwahoji wachangiaji na wasomaji wa gazeti la Pambazuko, ambao waliulizwa maswali matano makubwa, mengine yakiwa ni maswali madogo.

Maswali hayo yaliyotumwa kwa njia ya dodoso pepetevu (soft questionnaire) kupitia WhatsApp, yalikuwa haya: je, serikali imefanya kazi zake vyema kuhudumia wananchi kwa mwaka mmoja uliopita? Nini kifanyike ili maisha ya watu yawe bora zaidi? Je, serikali imegusa vipi maisha ya Mtanzania mmoja mmoja? Kama serikali imekwama, shida iko wapi na nini kifanyike? Na, unaiona Tanzania ikisimama wapi katika kipindi cha miaka 10 kutoka sasa?

Watu 412 walirudisha majibu yao na baadaye kufanyiwa uchambuzi wa kina. Watu walioshiriki zoezi ni wanaume 367, sawa na asilimia 89, wakati wanawake walikuwa 45, sawa na asilimia 11.

Asilimia 92 (sawa na watu 379) ya walioulizwa wamebainika kutoka Dar es Salaam. Waliobaki, yaani asilimia 8, sawa na watu 33, wako mikoa mbalimbali, na wachache walitoka nje ya Tanzania. Dodoso hilo halikuuliza umri wala elimu.

Watu 177, sawa na asilimia 43, wamekuwa na shaka kuhusu Tanzania kuwa na uchumi wa juu ndani ya miaka 10 ijayo. Wanaeleza wasiwasi wao kwa kuangalia zaidi matumizi ya serikali waliyoita "makubwa mno."

Hawa wanaeleza kwamba serikali kununua magari ya kifahari kila mwaka kwa mawaziri, manaibu, wakurugenzi, wakuu wa mikoa, wakuu wa wilaya, wakuu wa idara na taasisi, ni "kufuru" kwa walipa kodi.

Mmoja wa wajibu dodoso, ambaye ni kiongozi mstaafu alipiga simu kwa Pambazuko na kutoa dukuduku lake kwamba kwa nini magari makubwa na

*Inaendelea Uk. 11*

# Tanzania miaka 10 ijayo

aghali zaidi yanunuliwe wakati kuna barabara nzuri zaidi kwa sasa?

"Zamani wakati wa Mwalimu (Nyerere - rais wa kwanza- 1961 hadi 1985) wakubwa waliokuwepo walitumia magari ya kawaida sana, wakati hakukuwa na barabara nzuri, iweje hawa wa leo wajione ni bora zaidi na kujinunulia magari ya bei mbaya," amelalamika na kuongeza; 'hivi hawajua kuwa walipa kodi wanaumia." Pambazuko halitamtaja jina lake.

Waziri wa Fedha na Mipango Dkt. Mwigulu Nchemba amebainisha kuwa serikali kwa mwaka huu wa fedha itatumia Sh. bilioni 558 kununua magari.

Kiasi hiki, endapo nusu yake ingetumika kuagiza magari ambayo ni nafuu kidogo – hasa Prado, na inayobaki kujenga miundombinu ya barabara, kungepatikana barabara ya kiwango cha lami yenye urefu wa kilomita 233. Kilomita moja ya barabara hujengwa kwa Sh. bilioni 1.2.

Urefu huo ni sawa na umbali wa kutoka Mwanza hadi Bariadi (kilomita 230) au kutoka Njombe hadi Songea (kilomita 237).

Viongozi wakubwa serikalini hutumia magari yanayouzwa kuanzia Sh. milioni 250 hadi 330 na sheria hulazimisha magari kununuliwa mapya kutoka kwa mtengenezaji. Aina ya magari hayo ni Toyota LandCruise V8 na VX. Toyota Prado huuzwa nusu ya bei hizo.

Zaidi sana, hawa wenye matumaini finyu, wanaeleza kwamba rushwa na ubadhirifu vimeongezeka kiasi cha kutishia hayo matumaini ya kuwa na uchumi imara na maisha bora baada ya miaka 10 kuanzia sasa.

Wenye matumaini ya kuwa na maisha bora zaidi katika kipindi cha miaka 10 ijayo wanaeleza kuboreshwa kwa huduma za afya ni chahu, kwamba huenda bajeti kubwa ya fedha inayotengwa kwenye afya, ikasaidia kuimarisha afya, hivyo kuwa na nguvu kazi imara.

Kwamba endapo serikali itaendelea kuongeza bajeti ya afya, kuwa na madaktari wa kutosha, dawa na vifaa tiba, pamoja na vile vya uchunguzi, idadi ya watenda kazi wenye siha njema itaongezeka, hivyo kuwa na uhakika wa ongezeko la uzalishaji wa viwandani, ofisini na hata mashambani.

Katika bajeti ya 2022/23, serikali ilitenga jumla ya Sh. 1,109,421,722,000 ikiwa ni ongezeko la asilimia saba (sawa na Sh. 75,287,427,000) kutoka bajeti ya mwaka 2021/22 iliyokuwa Sh. 1,034,134,295,000, huku Rais Dkt. Samia akieleza mara kadhaa kwamba serikali itaendelea kuongeza bajeti hiyo.

**Utawala bora**

Katika kipindi cha miaka 10, Rais Samia atakuwa amestaafu utumishi wake wa umma – kwa nafasi ya urais kwani anatarajiwa kustaafu baada ya kutimiza awamu mbili za uongozi kikatiba. Atastaafu Novemba 2030 ikiwa atachaguliwa kuongoza kwenye uchaguzi mkuu wa 2025.

Katiba ya Tanzania inaharamisha rais yeyote kuzidisha awamu mbili za miaka mitano mitano, hata kama amefanya vizuri zaidi katika uongozi wake.

Kwa Rais Dkt. Samia, Watanzania hawatarajii kusikia mapambio ya wapambe kwamba "atake- asitake" – aendelee kuongoza hata baada ya awamu mbili kumalizika - kwani kufanya hivyo itakuwa ni kuvunja katiba ya nchi.

**Bado Dar au Dodoma?**

Mbali na kuwa dodoso pepetevu, Pambazuko pia lilifanya hojaji iliyohusisha sampuli ya kinasibu (random sampling) kutaka kujua Watanzania wanaiona wapi nchi yao kwa miaka 10 ijayo. Hili lilifanyika Wilaya ya Kinondoni, Dar es Salaam, pekee.

Miongoni mwa waliohojiwa ni Khamis Hamza, ambaye alieleza kuwa na elimu ya chuo kikuu. Alisema ana imani kuwa Tanzania ndani ya miaka 10 itakuwa mbali zaidi kiuchumi, kwamba mapato ya vijana wengi yataongezeka kutokana na

*Inaendelea Uk. 12*

# Tanzania miaka 10 ijayo

*Inatoka Uk. 11*

kukua kwa sekta ya viwanda.

Hata hivyo, kuhusu matumizi, akadai "serikali ina matumizi makubwa sana kwa sasa," na kuweka mfano mmoja kwa njia ya swali; "hivi ofisi za mawaziri na hata wakubwa wengine ziko wapi – Dar au Dodoma, wewe huwaoni wakipishana angani au barabarani kila wiki kuja Dar es Salaam?"

Anasema kupishana huko ni "pesa inateketea," hivyo akaongeza kwamba ni heri matumizi hayo ya safari za kila mara kwa viongozi wakuu zikapunguzwa – kwa wao kuishi zaidi Dodoma na fedha zaidi kuelekezwa kwenye maeneo mengine yanayogusa maisha ya Watanzania moja kwa moja.

**Uraia pacha**

Msomaji wa Pambazuko, Mtanzania anayeishi Kitongoji cha Coppell, Texas, Marekani anaandika kuwa Tanzania kuwa na uchumi imara zaidi na maisha bora kwa wengi ni kujidanganya kwani inaonekana kuwa na ubaguzi kwa raia wake, hasa wanaoishi na kufanya kazi nje ya nchi.

Anasema serikali inaendelea kupoteza fedha nyingi na fursa zinazoweza kupatikana kwa Watanzania walioko nje ya Afrika, hasa Marekani, kwani kuwanyima uraia ni "kujifunga kitanzi wenyewe."

Matamanio yake ni kwamba serikali ingeruhusu uraia pacha kama Kenya, Uganda, Afrika Kusini na nchi zingine jirani, ingekuwa na uhakika wa kuvuna, kile anachokiita "dhahabu kutoka Ulaya na Marekani." Anafafanua kwa kusema ni ujuzi na mitaji.

Mtanzania huyo, anaungana na wengine walioshiriki na kutamani serikali kuacha kile wanachoita "woga usiokuwa na sababu" na kuamua kuwa na uraia pacha.

**Uchumi utaimarika?**

Pambazuko limefanya mapitio ya taarifa mbalimbali za taasisi za kimataifa, Benki ya Dunia (WB), Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) na Benki Kuu ya Tanzania (BoT) kwa kipindi cha mwaka mmoja uliopita na kujiridhisha kwamba jitihada kubwa zinafanyika ili kuelekea kwenye uchumi imara.

Katika Fahirisi ya Ufanisi wa Kibiashara ya Benki ya Dunia (2021), nchi tano kati ya kumi zilizofanikiwa zaidi kukuza uchumi wake ziko barani Afrika, na theluthi moja ya mageuzi yote yaliyorekodiwa yalifanyika katika Afrika - kusini mwa Jangwa la Sahara. Tanzania inatajwa kuwemo.

Imebainika kwamba kuna ongezeko kubwa la uwekezaji wa nje ya nchi na kukomaa kwa wawekezaji wa ndani. Zaidi ya kampuni 100 ama zimeanza kazi au zimeomba leseni ya kuwekeza na tayari zimebanisha maeneo ya kuleta mitaji yao – Kampuni zote hizo zinaleta mtaji wa zaidi ya dola za Marekani trilioni moja.

Benki ya Maendeleo ya Afrika (ADB) inaeleza kuwa Tanzania ikiweka nguvu na utashi zaidi kwa kufanya maboresho ya kibajeti na kitaaluma, hasa katika sekta za nishati, kilimo, maji na madini, uchumi wake utapaa zaidi na wananchi wake kuwa na maisha bora.

Dkt. Lenny Kasoga, mchumi na mhadhiri mwandamizi mstaafu anaeleza kwamba Tanzania itakuwa na uchumi imara endapo tu, uchumi hautaingiliwa na misimamo ya kisiasa.

Anasema Tanzania inaongoza kuwa na rasilimali nyingi kuliko mataifa mengi ya Afrika na Ulaya, lakini watu wake wengi masikini na ustawi wao unakwamishwa na siasa kuingilia kila kitu na hata uchumi.

"Bahati mbaya hata wasomi wa uchumi nao wameingiliwa na siasa, wamekuwa wauza siasa badala ya kuuza mizania ya uchumi; mchumi akiwa na mawazo ya siasa zaidi, basi ujue hakuna kitu," anasema msomi huyo aliyewahi kufundisha vyuo vikuu Marekani, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na maeneo mengine.

# 2023: Uwe mwaka wa Katiba Mpya

**Na Deusdedith KAHANGWA**

KAZI ya kutathmini maendeleo ya miradi, ukiwemo mradi wa kuendesha nchi, hufanyika kwa kugawanya kipindi cha kutekeleza mradi katika hatua mbalimbali.

Zipo tathmini fupifupi za muda kama vile wiki, mwezi, robo mwaka, theluthi ya mwaka, nusu mwaka, theluthi mbili za mwaka, robo tatu za mwaka, au mwaka mzima. Kisha, tathmini hufanyika kila baada ya hatua mojawapo, kwa mujibu wa sera za mradi.

Mwisho wa mwaka 2022 ni wakati mzuri wa kuangalia nchi ilikuwa katika hali gani mwanzoni mwa mwaka; kupiga hesabu ya mafanikio na upungufu katika kipindi cha mwaka mzima; na hatimaye, kupendekeza mipango mipya kwa ajili ya safari ya mwaka unaofuata.

Vyanzo muhimu vya taarifa kwa ajili ya kufanikisha kazi hii ni Mpango Mrefu wa Maendeleo ya Miaka 25 (2020-2025); Mpango Mrefu wa Maendeleo ywa Miaka 15 (2010-2025); Mpango Mfupi wa Maendeleo ya Miaka Mitano (2021-2025); na maudhui ya Katiba ya Tanzania (1977).

Vigezo vya kupima mafanikio kwa kila sekta ya maendeleo vimo kwenye Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2021-2025).

Sekta hizo ni kilimo; sayansi, tekinolojia na ubunifu; viwanda; madini; ujenzi; maliasili na mazingira; utalii; habari, michezo na Sanaa; huduma za fedha; uchumi wa baharini; biashara na viwanda; elimu; afya; maji; mipango miji na makazi ya watu; usalama wa chakula; hifadhi ya jamii; utawala bora; amani, usalama na utulivu wa kisiasa.

### Mazuri ya mwaka 2022

Katika mwaka 2022 Watanzania tumeshuhudia ongozeko la mafanikio katika kila sekta iliyotajwa hapo juu.



*Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan*

Serikali ya awamu ya sita, chini ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, imeirisha huduma za afya kutokana na ujenzi wa zahanati na vituo vya afya na hospitali; imefanya ujenzi wa miundombinu ya elimu ukiwemo ujenzi wa madarasa, maabara na nyumba za walimu; imetekeleza ujenzi wa miradi ya maji na ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya umeme.

Aidha, serikali imefanya kazi ya kuimarisha ushirikiano wa kimataifa na kuiwezesha Tanzania kunufaika na fursa mbalimbali zikiwemo biashara za kimataifa, misaada, mikopo yenye masharti (na isiyokuwa nayo) na kuhemea teknolojia na ujuzi.

Pia, serikali imesimamia utulivu wa kisiasa na kijamii, pamoja na kuboresha utawala wa sheria na utoaji wa haki. Na muhimu zaidi, wizara nyingi za serikali ya awamu ya sita zimejitahidi kubuni mipango ya maendeleo ambayo tunaweza kuitumia kutathmini utendaji wa serikali.

*Inaendelea Uk. 14*

# 2023: Uwe mwaka wa Katiba Mpya

**Mabaya ya mwaka 2022**

Lakini, pamoja na mafanikio hayo, kuna upungufu pia. Kuna ushahidi kuonyesha kwamba, mwaka 2022 umeacha majeraha kadhaa kwenye maisha ya baadhi ya watu.

Kwa ujumla, mwaka 2022 ulioambatana na mmomonyoko wa heshima, tunu, majukumu na haki za kibinadamu, katika ngazi ya ujenzi wa taifa.

Chini ya ibara ya 7(1) ya Katiba (1977), vyombo vya dola vyenye mamlaka ya kutekeleza madaraka ya utawala, kutunga sheria au madaraka ya utoaji haki, vinalo jukumu la kutekeleza malengo muhimu na misingi ya mwelekeo wa shughuli za serikali, kama zinavyotajwa kwenye ibara ya 8 hadi 11, chini ya sehemu ya pili ya sura ya kwanza ya Katiba (1977).

Ibara hizi zinasema kwamba, kwa kuwa Tanzania ni nchi inayofuata "misingi ya demokrasia na haki ya kijamii," hivyo basi, "lengo kuu la Serikali" litakuwa ni kupigania "ustawi wa wananchi."

Hii maana yake ni kwamba, "mamlaka ya nchi na vyombo vyake vyote vinawajibika kuelekeza sera na shughuli zake zote katika lengo la kuhakikisha" kwamba utu wa binadamu unaheshimiwa na kuthaminiwa; haki za binadamu zinaheshimiwa;

Vinapaswa kuhakikisha kwamba sheria za nchi zinalindwa na kutekelezwa; kwamba utajiri wa taifa unatumiwa kwa manufaa ya wananchi wote; na kwamba maendeleo ya uchumi wa taifa yanakuzwa na kupangwa kwa ulinganifu na kwa pamoja.

Vinapaswa kuhakikisha heshima ya utu inahifadhiwa na kudumishwa; raia wote; wake kwa waume, bila ya kujali rangi, kabila, dini au hali ya mtu wanapata nafasi zilizo sawa; na kwamba aina zote za dhuluma, vitisho, ubaguzi, rushwa, uonevu au upendeleo zinaondolewa



*Makamu wa Rais Dkt. Philip Mpango*

nchini.

Na vinapaswa kuhakikisha kwamba matumizi ya utajiri wa taifa yatilie mkazo maendeleo ya wananchi kwa kuondosha umaskini, ujinga na maradhi; na kwamba nchi inatawaliwa kwa kufuata misingi ya demokrasia na ujamaa.

Hata hivyo, ibara ya 7(2) ya Katiba (1977), inasema kuwa, malengo ya kisera yaliyotajwa kwenye Katiba (1977), chini ya ibara ya 6 hadi 11, "hayatatiliwa nguvu ya kisheria na Mahakama yoyote."

Kwa sababu hii, mwaka 2022, ibara ya 7(2) ya Katiba (1977) ilikuwa kikwazo kwa njia nyingi. Vyama vya siasa vya upinzani viliponyimwa fursa ya kuendesha "demokrasia" kwa njia ya mikutano ya hadhara vilitamani kwenda mahakamani kuishitaki serikali kwa ukaidi, lakini vikakwama.

Watanzania walipokabiliwa na mgao wa maji wakati Bahari ya Hindi iko umbali wa wastani wa kilometa moja kutoka milango ya nyumba zao, walitamani

*Inaendelea Uk. 15*

# 2023: Uwe mwaka wa Katiba Mpya

*Inatoka Uk. 14*

kwenda mahakamani kuishitaki serikali kwa uzembe, lakini wakakwama.

Watanzania walipokabiliwa na mgao wa umeme wakati Tanzania inavyo vyanzo vya maji ya kutosheleza mahitaji ya kila Mtanzania kwa mwaka mzima, walitamani kwenda mahakamani kuishitaki serikali kwa uzembe, lakini wakakwama.

Wananchi Mkoa wa Katavi wanaokabiliwa na upungufu wa umeme kwa sababu ya kutounganishwa kwenye gridi ya taifa tangu tupate uhuru, walitamani kwenda mahakamani kuishitaki serikali kwa uzembe, lakini wakakwama.

Baadhi ya wanavyuo wa elimu ya juu walipokosa mikopo kwa sababu kwamba huko nyuma walikuwa wanasomea kwenye shule zenye karo kubwa, hata bila kujali kwamba walikuwa wanasomeshwa na wasamaria wema wasiokuwepo tena, walitamani kwenda mahakamani kuishitaki serikali kwa ubaguzi, lakini wakakwama.

Kwa ufupi, ibara ya 7(2) ya Katiba (1977) ni kikwazo kikubwa kwa "ustawi wa wananchi" kutokana na kuwafunga mikono kila mara wanapotaka kuiwajibisha serikali yao kupitia jukwaa la kimahakama.

Na jambo baya zaidi ni kwamba, hata Rasimu ya Katiba iliyopendekezwa na Bunge la Katiba, imerithi kifungu hiki kwa kunakili chini ya ibara ya 20(2), japo Rasimu ya Katiba iliyopendekezwa na Tume ya Warioba ilikuwa imekifuta.

Hii maana yake ni kwamba, Rasimu ya Katiba iliyopendekezwa na Bunge la Katiba ilitumia mabilioni shilingi za walipa kodi, lakini ikashindwa kuwatetea walipa kodi.

**Wito kuelekea mwaka 2023**

Changamoto zilizotajwa hapo juu zinapaswa kufanyiwa kazi kubwa na ili kuwa na ustawi wa nchi, wenye dhamana ya nchi yao – wananchi, wahakikishiwe kwamba katiba mpya inapatikana ili kuongeza na kuhakikisha usawa na ustawi unaotakiwa.

Ni vyema mwaka huu mpya wa 2023, ukiwa mwanga wa kupatikana kwa katiba mpya, ambayo inaweza kuwa chachu ya maendeleo zaidi na uimara wa amani na utulivu.

Kwamba mwaka mpya uwe na kila aina ya dalili za kukua kwa demokrasia, kujali utu na kuzingatia haki za binadamu bila kuwepo kwa chembe ya uonevu.

Kunahitajika Katiba mpya inayofafanua kinagaubaga dhana ya "heshima ya utu" kwa kiwango ambacho hakitoi mwanya kwa mtu yeyote, au chombo chcochote cha serikali, kusigina heshima hii.

Lakini pia, ifahamike kuwa urefu wa kiegama cha haki na majukumu unategemea urefu wa kitako cha utu na kimo cha tunu za binadamu. Kwa hiyo, kunahitajika Katiba mpya yenye sura ya haki.

Kwa kuwa haki ni nyenzo za kulinda tunu za binadamu zilizotajwa, kunahitajika Katiba mpya inayofafanua haki za binadamu, pasipo kumfunga mikono mwananchi kwa kiwango kinachomzuia kudai hadi zake mahakamani pale zinapovunjwa na serikali.

Hapa wananchi wanataka kuona haki zinazohusu madai chanya, haki zinazohusu madai hasi, haki zinazohusu uhuru chanya, haki zinazohusu uhuru hasi, haki zinazohusu kibali cha kubadilisha haki za watu baki, na haki zinazohusu kizuizi cha kubadilisha haki za watu baki zinafafanuliwa vyema.

Mwaka huu mpya wa 2023, ukawe mwaka wa Katiba mpya yenye usawa na inayojali misingi na haki za binadamu.

# Maana ya utajiri kwa Elon Musk

**Na Mwandishi MAALUM**

TAJIRI nambari wahedi duniani, Elon Musk wa Marekani ana mtazamo wenye kustaajabisha kuhusu utajiri wake.

Anapendelea kuishi maisha ya upweke. Hapendi watu wengi wajue anakaa wapi. Haamini kuwa pesa ndiyo utajiri, pamoja na kwamba anazo nyingi.

Ingawa anachukia sana umasikini wa pesa na kutamani kila mmoja awe nazo za kutosha kuhudumia familia na kusaidia jamii yenye uhitaji.

Miaka michache iliyopita aliwahi kuuliwa swali ambalo majibu yake yanatoa mwanga juu ya mtazamo wake kuhusu utajiri.

**Swali:** Wewe ni tajiri zaidi duniani, je, unaweza kuruhusu binti yako kuolewa na kijana kutoka familia fukara?

**Jibu (Musk):** Kwanza kabisa, elewa kwamba utajiri haumaanishi kuwa na akaunti yenye fedha nyingi benki. Utajiri kimsingi ni uwezo wa kutengeneza mali…

… Mfano, mtu anayeshinda bahati nasibu au kamari. Hata akishinda milioni 100 siyo tajiri: Ni masikini mwenye pesa nyingi. Ndiyo sababu asilimia 90 ya mamilionea wa bahati nasibu wanakuwa masikini tena baada ya miaka michache…

… Pia ieleweke kuwa wapo matajiri ambao hawana pesa, mfano mzuri ni wajasiriamali wengi, hawa wapo njiani kuelekea kwenye utajiri japokuwa hawana pesa, maana wanakuza akili zao za fedha na huo ndio utajiri, hivyo nasema binti yangu anaweza kuolewa na kijana mwenye akili...

… Na pia lazima tuelewe tofauti ya tajiri na masikini ni ipi? Kwa maneno rahisi, tajiri anaweza kufa ili kuwa tajiri, na maskini anaweza kuua ili kuwa tajiri…

… Ukiona kijana anajifunza mambo mapya, na mwenye kiu ya kufahamu jambo hili na lile, na anathubutu kufanya jambo, tambua kuwa huyo ni tajiri…

… Ukiona kijana anafikiri kukwama kwa biashara ama ujuzi wake, mara zote tatizo ni serikali, na anayedhani kuwa matajiri wote ni wezi na anakosoa kila mara, ujue huyo ni masikini…


*Elon Musk*

… Tajiri wanaamini kwamba wanahitaji tu habari na mafunzo ili waweze kufanikiwa, masikini wanafikiri kwamba lazima wengine wawape pesa ili nao wafanikiwe…

… Hivyo, ninaposema kwamba binti yangu hataolewa na mtu masikini, sizungumzii kuhusu pesa. Naongelea uwezo wa kutengeneza mali ndani ya mtu huyo...

… Siku moja, mlinzi wa benki moja alikuta mfuko umejaa pesa umechwa tu mezani, akauchukua na kwenda kumpa meneja wa benki...

… Watu walimwita mtu huyu kichaa na mpumbavu, lakini ukweli mtu huyu alikuwa ni tajiri tu ambaye hakuwa na pesa...

Mwaka mmoja baadaye, benki ilimpa kazi ya kupokea wageni, miaka mitatu baadaye alikuwa meneja wa wateja na miaka 10 baadaye akawa mkuu zaidi na bonasi yake ya mwaka inazidi kiwango ambacho angeweza kuwa nacho kama angechukua fedha za watu.

# Pambazuko

## Gazeti la Pambazuko sasa kupokea matangazo

EWE mfanyabiashara na mtoa huduma, endapo unahitaji kuwafikia wateja wengi zaidi bila kujali mipaka ya eneo ulilopo, tangaza nasi kwa

kuwasiliana kupitia namba hii: **0744 768 263** au Barua- Pepe; info@pambazuko.tz

***Karibu sana Pambazuko isaidie kupaisha na kupambazua***

***huduma na biashara yako.***

# Je, Tanzania iko njia sahihi?

**Na Mwandishi WETU**

KAZI ya kuongoza nchi ni jukumu la kuongoza "mradi wa ujasiriadola" kwa kuzingantia kanuni za kawaida za uongozaji wa miradi inayobuniwa na binadamu.

Ni kazi ya kusimamia miradi mbalimbali; mradi wa ufugaji wa kuku, kilimo cha nyanya, ujasiriamali wa duka, au mradi wa kuendesha shule.

Zipo kanuni zinazounda pentagoni ya vigezo vikuu vitano. Kuna ubora wa matokeo ya mradi ambao hutegemea ukubwa wa bajeti iliyotengwa; muda wa kutekeleza mradi; uzito wa kazi inayotekelezwa; na upatikanaji wa rasilimali watu yenye weledi wa kusimamia, kutekeleza na kutahmini maendeleo ya mradi.

Katika mradi wa kuongoza nchi, mapokeo ya kidunia yanatufundisha kwamba, mwisho wa kila mwaka, na mwaka 2022 ukiwemo, unapaswa kuwa wakati wa kufanya tathmini ya maendeleo ya mradi wa kuongoza nchi.

Baadhi ya wakuu wa nchi husoma "Hotuba Kuhusu Hali ya Maendeleo ya Nchi." Na wachambuzi wa masuala ya kisiasa hufanya uchambuzi kama huo, wa kupima kilichovunwa baada ya mwaka mmoja.

Katika uchambuzi wa aina hii, mchambuzi huangalia nchi ilikuwa katika hali gani mwanzoni mwa mwaka; hupiga hesabu ya mafanikio na upungufu katika kipindi cha mwaka mzima; na hatimaye, mchambuzi hupendekeza mipango mipya kwa ajili ya safari ya mwaka unaofuata.

Katika ngazi ya taifa, mwongozo wa tathmini ya Maendeleo ya Tanzania unaweza, na unapaswa, kupatikana kwenye maudhui ya Mpango Mrefu wa Maendeleo ya Miaka 25 (2020-2025); Mpango Mrefu wa Maendeleo ya Miaka 15 (2010-2025); Mpango Mfupi wa Maendeleo ya Miaka Mitano (2021-2025); na maudhui ya Katiba ya Tanzania (1977).



*Uchumi unakua*

Katiba ya Tanzania (1977) inataja mambo makuu matano, yaani tunu za taifa; malengo makuu ya kitaifa, misingi ya mwelekeo wa shughuli za serikali na sera za taifa katika sekta mbalimbali za maisha; haki za watu; majukumu ya msingi; na mipaka ya haki na majukumu husika.

Andiko la Mpango wa Maendeleo wa Miaka 25 (2020-2025) linaonyesha kuwa, ifikapo mwaka 2025, Dira ya Tanzania ni kuwa nchi yenye uchumi wa viwanda utakaoifanya kuwa nchi yenye ukuaji endelevu wa pato la Taifa kama zilivyo nchi za uchumi wa kati.

Je, tukiwa tumebakiza miaka miwili kufikia mwisho wa dira hiyo, Tanzania inaelekea kwenye njia inayofaa kufikia huko, au haisogei?

Na kama haisogei nini kifanyike, na endapo inasogea, je, kasi yake inaweza kufikisha nchi huko ilikojiwekea kufika kwa muda huo?

Je, katika mwaka 2022, serikali ya awamu ya sita, chini ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, imefanya vizuri wapi na kujikwaa wapi?

**Tafakari**

## Tuongeze bidii 2023

**Mhariri,**

**H**ALI ya ugumu wa maisha kwa mwaka ulioisha, 2022 ilionekana zaidi na kuibua malalamiko kila kona ya nchi yetu.

Malalamiko haya hayakuwa bure, uhakika ni kwamba maisha yalikuwa magumu kila kona; iwe mijini na vijijini ndiyo kabisa, hali ilikuwa tete.

Mijini bei za vyakula zilionekana kuwa kubwa na zikaendelea kupanda siku hadi siku. Gharama za maisha zikaongezeka na hali ya uchumi kuwa ngumu.

Vijijini hali kadhalika, hakuna mvua na kufanya mazao ya vyakula kuwa adimu. Hivyo, ugumu wa maisha.

Pamoja na kwamba huenda hali ikawa namna hiyohiyo kwa mwaka huu mpya, kutokana na kukosekana kwa mvua na mambo mengine, ikiwamo vita vya Russia na Ukraine, lakini bado tunapaswa kupeana shime, kwamba kila mmoja aongeze bidii kwa kazi ambazo anafanya.

Bidii zaidi inaweza kutuhakikishia kipato zaidi, na kuwa na nguvu ya uchumi kukabili mfumuko wa bei ambao unaonekana kushika kasi.

***Heri ya mwaka mpya 2023.***
***Khamis Jumanne,***
***Mbagala- Rangi Tatu***

## Naomba kujua afya ya Dk. Salim

**Mhariri,**

**M**IMI ni kijana ambaye nampenda sana aliyekuwa waziri mkuu wa Tanzania miaka iliyopita, Balozi Dkt. Salim Ahmed Salim.

Sijamuona siku nyingi mbele ya umma na hivyo kuwa na wasiwasi wa uimara wa afya yake. Naomba kujua yuko wapi na afya yake ikoje?

***William Magosi***
***Email: masosiwilly@gmail.com***

**Jibu:**

Pambazuko limezungumza na kijana wake, Ahmed kuhusu hali ya afya ya Dkt. Salim ambaye amesema baba yake anaendelea vyema pamoja na kukabiliwa na changamoto ya afya.

Dkt. Salim pia wiki iliyopita alionekana akiwa ametembelewa na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa nyumbani kwake Masaki, Dar es Salaam.

***Mhariri.***

## Hongereni Pambazuko

**Mhariri,**

**P**AMOJA na kukutakia heri ya mwaka mpya – 2023, napenda kupongeza timu nzima ya wahariri, waandishi, wachangiaji na watendaji wengine wa gazeti lako.

Hakika mmekuwa mkitupatia taarifa, elimu na maarifa mengi zaidi kuliko chombo chochote cha habari kwa sasa Tanzania.

Kazi mnayofanya ni yenye ubunifu mkubwa na zaidi sana tunapata huduma hii bila kulazimika kutoa pesa.

Tunaomba mwaka kesho muongeze kurasa na habari za vijijini, kama itawezekana ili kutupa maarifa mengi zaidi.

**Joseph Maige,**
**Kahama.**

**Mhariri:** Aksante sana Joseph kwa pongezi zao, zimefika kwa wahusika. Kuhusu kuandika habari za vijijini, ni kwamba tutafika, ingawa kwa sasa tunakwamishwa na fedha za kufanya kazi hiyo, maana bado tunafanya kazi hii ya kuupa umma maarifa, taarifa na mengineyo kwa kujitolea – bure kama ambavyo tunakufikia bure.

### *Tunapokea Barua*

***Mhariri anapokea barua kutoka wasomaji wake kwa ajili ya kuzichapisha ama kuzitafutia majibu kutoka ofisi za serikali na binafsi. Tuma barua yako kwa njia ya barua-pepe: info@pambazuko.tz au kupitia namba ya simu: 0744 768 263***

# Nafasi ya sheria kujenga nchi

**Na Deusdedith KAHANGWA**

TUNAPOANZA mwaka mpya wa 2023, kuna umuhimu wa kukumbushana kuhusu tofauti kati ya sheria za maadili na sheria za bunge ili tuweze kuendesha nchi vizuri zaidi.

Hivyo, najadili "misingi ya utawala wa sheria" kwa kujibu swali lifuatalo: "sheria ni kitu gani na siyo kitu gani?" Marejeo yangu ni sura ya tatu ya kitabu cha Profesa John Stuart Mackenzie wa Uingereza, "A Manual of Ethics." Huyu ndiye mwanafalsafa wetu wa wiki.

Awali ya yote, napenda kusema kuwa, sheria ni tamko linalosema angalau jambo moja kati ya mambo matatu yafuatayo:


Ama ni tamko linaloeleza hali ya mambo ilivyo au mchakato fulani unavyotokea (description); Au ni tamko linaloeleza kitendo kinachopaswa kufanyika au kinachopaswa kutofanyika, na likikiukwa, kuna ushauri nasaha unafuata (prescription);

Au ni tamko linaloeleza kitendo ambacho lazima kifanyike au lazima kisifanyike, na likikiukwa kuna adhabu inafuata (obligation).

Kwa ujumla, sheria yoyote iwayo inaweza kuwa na sifa zifuatazo: ama inaweza kubadilika au haiwezi kubadilika; ama inaweza kukiukwa au haiwezi kukiukwa; ama inawahusu watu wote au inawahusu watu wa eneo moja pekee.

Lakini, mara nyingi, sheria inayowahusu watu wote pia ni sheria isiyobadilika, na sheria inayolihusu eneo maalum pia ni sheria inayoweza kubadilika.

Kwa kutumia sifa hizi, tunaweza kuwa na aina nne tofauti za sheria. Kuna sheria zinazoweza kubadilika na zinazoweza kukiukwa, sheria zinazoweza kubadilika na zisizoweza kukiukwa, sheria




zisizoweza kubadilika na zinazoweza kukiukwa, na sheria zisizoweza kubadilika na zisizoweza kukiukwa. Tutazijadili hatua kwa hatua.

Mosi, "sheria zinazoweza kubadilika na zinazoweza kukiukwa" ni pamoja na sheria zinazotungwa na familia, koo, makabila, mabunge, mabaraza ya madiwani, na mabaraza ya maendeleo ya kata.

Wanadamu, wanaweza kukiuka sheria za nchi zao. Lakini sheria zinasema kwamba hawapaswi kufanya hivyo. Hivyo, zinaambatanisha adhabu kwa wakiukaji. Hivyo, zinaweza kubadilishwa na kuvunjwa.

Pili, "sheria zinazoweza kubadilika na zisizoweza kukiukiwa" ni pamoja na sheria za kiuchumi, kama sheria ya ugavi na utashi. Sheria inaeleza jinsi bei za bidhaa zinavyobadilika kulingana na kiwango cha mahitaji na ugavi.

Bei hazikiuki na haziwezi kukiuka sheria za kiuchumi, mradi tu hali zinazofaa za kijamii hazibadiliki. Lakini, sheria za kiuchumi zitabadilika ikiwa, tuseme, tabia za watumiaji wa bidhaa zitabadilika.

Pia, chini ya kundi hili la sheria tunazo

*Inaendelea Uk. 21*

# Nafasi ya sheria kujenga nchi

*Inatoka Uk. 20*

sheria za hisabati. Zinatueleza ni kitendo gani kinaweza kufanywa kwenye namba gani, na matokeo tarajiwa ni yapi. Kuna matendo ya kugawanya, kuzidisha, kujumlisha, kutoa.

Matendo haya hayakiuki na haziwezi kukiuka sheria za hisabati, mradi tu mazingira stahiki ya kihisabati yasibadilike. Lakini, sheria za hisabati zitabadilika ikiwa mfumo wa nambari utabadilika.

Kwa mfano, katika ulimwengu wa hisabati unaotumia kizio cha kumi, mbili kujumlisha tatu ni tano, wakati katika ulimwengu wa hisabati unaotumia kizio cha tano, mbili kujumlisha tatu ni kumi.

Tatu, "sheria zisizoweza kubadilika na zinazoweza kukiukwa" ni pamoja na sheria za asili za maadili asilia. Sheria za maadili husema jambo ambalo linapaswa kufanyika. Ukiukwaji wake hauambatani na adhabu kali kama ilivyo kwa sheria za Bunge.

Mifano ya sheria za maadili ni pamoja na: unapaswa usiue, usiibe, usiseme uwongo, usile rushwa, usijeruhi mwili wa mtu, na usiharibu mazingira; unapaswa kufanya kazi kwa bidii, kutetea uhai wa mtu asiye na hatia.

Sheria hizi hazibadiliki, ingawa zinaweza kuvunjwa. Ni kanuni pana zinazowahusu watu wote wenye akili timamu.

Mfano mwingine chini ya kikundi hiki cha sheria ni sheria zinazohusu taratibu za usanifu wa majengo, ujenzi, utoaji hotuba na kanuni za mantiki.

Mfano wa mwisho chini ya kipengele hiki ni sheria za Mungu kama zilivyofunuliwa katika misahafu mbalimbali, kama vile "Amri Kumi," katika maandiko ya Kikristo na Kiyahudi.

Na nne, "sheria zisizoweza kubadilika na zisizoweza kukiukwa" ni pamoja na sheria asilia za kifizikia kama vile sheria za mfumo wa jua, mchana na usiku, majira ya kupanda na kuvuna.

Sheria asilia za kifizikia pia zinajumuisha misimu mbalimbali ya kijiografia, na sheria ya uvutano, ambayo husema tu kwamba kati ya magimba mawili kuna nguvu ya uvutano inayotegemea uzito na umbali kati ya magimba hayo.

Sheria asilia za kifizikia ni kanuni za jumla kuhusu kile kinachotokea kila mara. Zinaeleza matukio asilia yanarudia mara kwa katika mazingira fulani.

Sayari hazibadilishi na haziwezi kubadilisha sheria asilia za kifizikia, mradi tu mazingira stahiki ya kijiografia yaendelee kuwepo.

Lakini, sheria asilia za kifizikia zinaweza kubadilika ikiwa hali fulani katika mfumo wa jua itabadilika, mfano, kupoa kwa jua, kupungua kwa kasi ya dunia, au dunia kugongana na nyota fulani, na hivyo kuhama njia.

Kundi hili la sheria pia linajumuisha kanuni za meriolojia, kama vile, kitu kizima ni kikubwa kuliko sehemu yake yoyote; na sheria za etiolojia, kama vile, kila tukio linayo sababu yake.

Kwa muhtasari, basi, tumeona kwamba, sheria ni tamko linalosema angalau jambo moja kati ya mambo matatu yafuatayo:

Ama ni tamko linaloeleza hali ya mambo ilivyo au mchakato fulani unavyotokea; Au ni tamko linaloeleza kitendo kinachopaswa kufanyika au kinachopaswa kutofanyika;

Au ni tamko linaloeleza kitendo ambacho lazima kifanyike au lazima kusifanyike. Pasipo utekelezaji adhabu itolewe.

Kwa mantiki hiyo basi, ni vyema sana mwaka huu sheria za nchi zikasimamiwa vyema ili kuwa na Tanzania tunayoitamani.

# Lala salama Pele



**Na Mwandishi WETU**

BAADA ya kupata taarifa za kifo cha gwiji la soka duniani, Diego Maradona – Novemba 25, 2020, mfalme wa kandanda, Edson Arantes do Nascimento – almarufu Pele alisema; "alale salama Maradona, tutakutana mbinguni baadaye."

Sasa safari yake imetimu. Aliondoka juu ya uso wa dunia Desemba 29, mwaka huu na huenda ameelekea huko alikoeleza atakutana na Maradona.

Pele (82), raia wa Brazil amekuwa nembo ya viwango vya ubora wa mchezo huo kwa miaka yote na kuendelea kupewa sifa hizo hadi anafariki dunia wakati akiendelea na matibabu katika hospitali ya Albert Einstein mjini Sao Paulo, Brazil. Alikuwa akisumbuliwa na saratani ya utumbo.

Anasifiwa kwa kufunga mabao 1,281 katika rekodi ya dunia katika mechi 1,363 katika kipindi cha miaka 21 ya maisha yake, yakiwemo mabao 77 katika mechi 92 za nchi yake.

Pele ndiye mchezaji pekee aliyeibeba timu ya Brazil kushinda Kombe la Dunia mara tatu, akinyakua taji hilo mwaka 1958, 1962 na 1970.

Kutokana na umahiri, kujituma, nidhamu, Pele alitangazwa kuwa Mchezaji Bora wa Karne wa Shirikisho la Soka Duniani (Fifa) mwaka 2000.

Afya ya mfalme huyo wa soka ilianza kutetereka mika amiwili iliyopita baada ya kugundulika kuwa na matatizo ya figo, lakini baadaye madaktari wakaeleza kuwa amekumbwa na saratani ya utumbo mpana.

Pele alifanyiwa upasuaji wa kuondoa uvimbe kwenye utumbo wake Septemba 2021 katika hospitali hiyohiyo alipokutwa na umauti.

Alhamisi iliyopita, binti yake alichapisha picha ya kile kilichoonekana kuwa mikono ya familia ya Pele kwenye mwili wake hospitalini na kuandika: "Kila kitu tulicho ni shukrani kwako. Tunakupenda sana. Pumzika kwa amani."

Edson Arantes do Nascimento, anayejulikana zaidi kama Pele, alikua nyota wa kimataifa alipokuwa na umri wa miaka 17, alipoisaidia Brazil kushinda Kombe la Dunia la 1958 nchini Uswisi, na kulazimisha kuingia kwenye safu ya kuanza kwa hatua ya mtoano.

Alifunga bao pekee katika ushindi wa 1-0 dhidi ya Wales katika robo fainali, 'hat-trick' dhidi ya Ufaransa katika nusu fainali na mawili katika ushindi wa 5-2 dhidi ya wenyeji – Uswisi kwenye fainali.

***Alale salama Pele.***

# Ni Samia au tusubiri ajaye?

**Na Shabaan LULELA**

TANZANIA imekuwa – miaka nenda rudi- ikitamani kushiriki fainali kubwa kabisa duniani kwa mchezo wa kandanda – Kombe la Dunia bila kuwa na mipango madhubuti na hata ile inayowekwa, haitekelezwi kwa kiwango.

Kupitia kwa mawaziri wenye dhamana ya michezo au kiongozi wa nchi, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imekuwa ikitangaza kwamba "inaweza kushiriki fainali hizo."

Kimsingi, kinafanyika ni "utashi unaosukumwa na siasa zaidi" badala ya kujenga mfumo wenye mantiki ya kuhakikisha matamanio hayo yanafikiwa.

Muasisi wa Tanzania, Mwalimu Julius Nyerere hakuwa mpenzi wa kandanda, na hadi anang'atuka madarakani hakuupa mchezo huo nafasi kubwa, na hakuonekana kuufuatilia kwa kiwango kikubwa.

Aliyemfuatia kuanzia 1985 hadi 1995, Rais Ali Hassan Mwinyi, naye kama alivyokuwa mtangulizi wake, hakuwa shabiki sana, ingawa alimzidi kidogo Mwalimu Nyerere, angalau kwa kutambua kuwepo timu kadhaa, ukiacha Simba, Yanga; Coastal Union, Nyota Nyekundu na zinginezo.

Rais aliyemfuatia Mwinyi kuanzia 1995 hadi 2005, Benjamin Mkapa, naye hakuwa na tofauti kubwa na wote wawili, ingawa aliweka juhudi zake kuhakikisha uwanja mkubwa wa michezo unajengwa – Uwanja wa Mkapa, Dar es Salaam.

Miaka 10 baadaye, akaingia Rais Jakaya Kikwete. Huyu akaonyesha nia ya dhati; akaleta kocha wa kigeni ambaye alihudumiwa na serikali, akatenga fungu la fedha la kueleweka kuendesha timu ya soka ya taifa (Taifa Stars).

Ni Kikwete alipandisha ari kwamba Tanzania inaweza kuwa tishio, lakini naye hakufika mbali, maana alikuwa na wasaidizi wasiopenda mpira. Hawakusaidia. Waligeuza michezo kuwa eneo linaloweza kuitwa "chumio binafsi."



*Kombe*

Kuanzia 2015 hadi 2021, aliingia Rais John Magufuli, huyu naye hakuonekana kupenda mpira, zaidi ya kuuchukulia kuwa sehemu ya kupata alama zaidi katika siasa zake. Akajielekeza kuwa yeye ni shabiki wa timu zote; zaidi akizitaja Simba na Yanga. Hata akivaa jezi yenye utambulisho wa timu zote mbili. Jezi moja yenye Simba na Yanga hapohapo. Ajabu!

Sasa Tanzania ina kiongozi wa awamu ya sita - mwanamama, Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan. Huyu hajui masuala ya mpira, ingawa anaweza kuzitaja baadhi ya timu za daraja la kwanza.

Ieleweke kuwa Tanzania haijawahi kushiriki Fainali za Kombe la Dunia tangu ilipojiunga na Shirikisho la Soka la Kimataifa (FIFA) mwaka 1964, lakini imewahi kushiriki Fainali za Mataifa ya Afrika (Afcon) mwaka 1980 zilizofanyika Nigeria na 2019 zilizofanyika Misri.

**Nani atufukishe Kombe la Dunia? Ni Rais Samia au tusubiri mwingine?**

# TUENZI ASILI YETU...



*Mwanahabari nguli Jenerali Ulimwengu akiwa na mkewe, Josephine wakifurahia kinywaji cha asili ya Kabila la Wachaga; mbege - huko Kijiji cha Lyamrakana, Marangu, Moshi Vijijini mkoani Kilimanjaro - Desemba 27, 2022. Familia ya Ulimwengu ilisafiri kwenda kijijini kwa mapumziko ya mwisho wa mwaka. Tuendelee kuenzi utamaduni wetu kwa kupenda mila zetu, ikiwamo vinywaji vya asili badala ya "kuviponda." (Picha kutoka kwa familia).*

*GAZETI hili huandaliwa na kusambazwa na Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (Tampa). Pambazuko limesajiliwa na Serikali ya Tanzania, kupitia Idara ya Habari (MAELEZO) na kupewa leseni namba - 00000448.*

TAMPA
TANZANIA MEDIA PRACTITIONERS ASSOCIATION